# KISWAHILI MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KIDATO CHA 1

**2. UFAHAMU** MWONGOZO WA KUSAHIHISHA.

***Soma taarifa ifuatayo halafu ujiu maswali***

***UMOJA NA UTANGAMANO WA KITAIFA***

Taifa ni jamii ya watu wanaoishi pamoja na kuunganika kihistoria na kitamaduni chini ya serikali moja. Muunganiko huu hutokea kinasibu na watu kujikuta chini ya himaya moja. Umoja na utangamano katika taifa hutokana na mambo kadha wa kadha.

Kwanza kabisa ni ushirikiano baina ya wanajamii wenyewe. Umoja wao huletwa na lugha wanayotumia. Hapa nchini Kenya Kiswahili kimechangia pakubwa katika kuleta utangamano. Luhga ya Kiswahili inazungumzwa kote nchini. Wananchi kutoka sehemu tofauti za nchi wanaweza kuwasiliana bila shida yoyote.

Pili, utawala wa serikali ya kitaifa huleta utangamano wa jamii katiak nchi. Huduma za serikali hutolewa kwa wote bila y aubaguzi. Nchi inapokuwa chini ya kiongozi aliyechaguliwa na wananchi hufanikisha umoja.

Jambo linguine ambalo huleta utangamano wa kitaifa, ni kuweko kwa sera inayoongoza maazimio na malengo ya taifa. Viongozi na wananchi wote hujitahidi kuchangia katiak kuyafikia maazimio na malengo ya taifa lao.

Utamaduni wan chi nao ni muhimu katika kuleta umoja wa kitaifa. Mila, itikadi na kaida zenye manufaa na zinazokubalika na jamii hufanikisha kutambulisha taifa. Hivyo wananchi kupigania kwa jino na ukucha kuhifadhi utamaduni wao. Kwa mfano: sanaa za uigizaji na uimbaji nchini Kenya husaidia kutomelea umoja huu. Tamasha hizi ni chombo muhimu cha utangamano. Mfumo sawa wa elimu nchini ni jia nyingine ya kuimarisha umoja wa kitaifa.

Wafanyibiashara wanaposafiri kutoka sehemu moja ya nchi had nyingine hutangamana na wananchi wenzao wanapouza au kununua bidhaa na huduma. Utangamano huo hukuza umoja wao.

***Maswali***

a) Eleza maana ya taifa. (al 2)

Taifa ni jamii ya watu wanaoishi pamoja na kuunganika kihistoria na kitamaduni chini ya serikali moja.

b) Eleza umuhimu wa Kiswahili nchini Kenya. (al2)

Kiswahili kimechangia katika kuleta moja na utangamano.

c) Taj amambo manne ambayo huleta umoja wa kitaifa. (al4)

i) Lugha inayotumiwa na jamii.
ii) Utawala wa serikali.
iii) Sera inayoongoza maazimio na malengo ya taifa.
iv) Utamaduni wa nchi.

...................................................................................................................................

...................................................................................................................................

...................................................................................................................................

...................................................................................................................................

d) Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mujibu wa kifungu hiki. (al 2)

i) Utangamano....Maingiliano, mahusiano.

ii) Utamaduni ....Mila, desturi. imani....

**3. *Matumizi ya lugha (al. 30)***

a) Taja sifa mbili mbili za sauti zifuatazo. (al. 4)

i) /u/...Irabu ya nyuma Kati, midomo huwa imeviringwa.

ii) /e/...Irabu ya Mbele Kati, midomo hutandazwa

b) Yaja sauti mbili mbili ambazo ni, (al. 6)

i) Vipasuo..../p/, /b/, /t/, /d/, /k/ /g/.......

ii) Nazali..../m/, /n/, /ny/, /ng'/...................

iii) Vikwamizo......................................................

c) Pambanua ain aza maneno katika sentensi ifuatayo. (al. $2^1/_2$)

Maharagwe yalivunwa na kutiwa ghalani.

.....Maharagwe – Nomino, Yalivunwa – Kitenzi, na – Kihusishi, Kutiwa – Kitenzi ghalani – Kielezi cha Mahali..

d) Panga maneno haya vizuri ili yaunde sentensi sahihi. (al. 2)

Hodari Yule mwanamuziki nchi amezuru nyingi Afrika za.

.....Yule Mwanamuziki hodari amezuru nchi nyingi za Afrika.

e) Tunga sentensi moja moja kubainisha maana ya maneno yafuatayo; (al.2)

i) Paa – Kwenda juu
- Mnyama – Mbuzi Mwitu
- Sehemu ya juu ya nyumba

} Hakiki Sentensi ya Mwanafunzi.

ii) Shuka – Kuteremka kutoka juu.
- Kitambaa cha kutandika Kitandani

(Kadiria Sentensi ya mwanafunzi).

f) Kanusha sentensi ifuatayo; (al. 2)

Mwalimu anasahihisha kitabu cha mwanafunzi.

.....Mwalimu hakusahihisha Kitabu cha Mwanafunzi.

g) Andika sentensi ifuat ayo upya ukizigatia maagizo kwenye mambano. (al. 2)
Mazingirta yamehifadhiwa. (hali ya mazoea)

Mazingira huhifadhiwa.

h) Maneno yafuatayo hupatikana katika ngeli zipi? (al. 2)

1. Manukato....YA-YA....

2. Sukari....I-I....

i) Tofautisha sentensi hizi. (al. 4)

1. Gari liliibwa

Gari lote limechukuliwa na Mwizi.

2. Gari liliibiwa

Sehemu ya gari imechukuliwa.

j) Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia vitenzi vilivyo katakia mambano.(al. 2)

i) Sauti hii ili Shonwa na fuudi wa kihindi. (shone)

ii) Yuko wapi Yule mgonjwa aliyeletwa hapa? (leta)

k) Eleza maana ya msamiati ufuatao wa ushairi. (al. $2^1/_2$)

i) Ubeti

Ni aya au Stanza ya Shairi.

ii) Mizani

Ni silabi/mapigo yanayounda Maneno ya Shairi.

iii) Mshororo

Ni Mstari wa Shairi (ubetini)

iv) Ukwapi

Kipande cha Kwanza Katika Mshororo wa Shairi.

v) Dhamira - Lengo/Kiini/Kusudi/madhumuni ya Kufanya jambo.

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

**4.ISIMUJAMII (al 10)**

a) Eleza maana ya;

i) Isimu

✓ Ni sayansi ya lugha.

✓ Ni taaluma inayochunguza lugha kisayansi

iii) Jamii

✓ Ni kundi la watu wanaoishi na kuendesha shughuli zao pamoja.

iv) Isimujamii

✓ Ni matumizi ya lugha katika jamii.

✓ Ni taaluma inayochunguza uhusiano baina ya lugha na jamii

v) Sajili

✓ Ni matumizi ya lugha katika muktadha fulani.

✓ Ni namna mbalimbali lugha inatumika ~~katika~~ muktadha ya jamii.

vi) Lafudhi

✓ Ni upekee wa mtu kimatamshi kutokana na athari za lugha ya kwanza.

✓ Ni tofauti kimatamshi kwa wazungumzaji wa lugha moja.

**5.FASIHI SIMULIZI. (al 10)**

a) Eleza maana ya fasihi. (al. 2)

✓ Ni sanaa inayotumia lugha kuchambua vipengele mbalimbali vya maisha ya binadamu.

b) Toa sifa nne ili kutofautisha fasihi andishi na fasihi simulizi. (al. 8)

| Fasihi Andishi | Fasihi Simulizi. |
|---|---|
| 1. Ni mali ya mtu binafsi | 1. Ni mali ya jamii nzima. |
| 2. Inahifadhiwa vitabuni. | 2. Inahifadhiwa akilini. |
| 3. Si rahisi kubadilishwa | 3. Ni rahisi kubadilishwa. |
| 4. Huwa na hadhira lengwa | 4. Haina hadhira mahususi. |
| 5. Hadhira yake ni tuli | 5. Hadhira yake ni tendi/hai. |
| 6. Hugharimu wakati na pesa. | 6. Haina gharama. |
| 7. Ubora wake hutegemea ujuzi wa mwandishi. | 7. Ubora wake hutegemea ujuzi wa fanani. |